MTANDAO WA KUZUIA UKATILI WA KIJINSIAG

**Siku 16 za Unaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia 2017**

**Mwongozo wa Shughuli za Kampeni**

# KILA MSICHANA ANA THAMANI!

JE! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

## KILA MSICHANA ANA THAMANI! JE! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

Tunayofuraha kwa wewe kujiunga na mamia ya wanaharakati kwenye kanda hii ili kuhakikisha wasichana wanapata elimu. Kwa hatua hii unaweza kufikiria juu ya shughuli utakayo iendesha' chapisho hili litakusaidia kutambua na kupanga kwa sababu litakupa maelezo ya jumla ya shughuli unazoweza kuzifanya pamoja na hatua za maandalizi. Pia utapata maelezo ya shughuli mbalimbali za kijamii na wanahabari. Tunakuhamasisha kufanyia kazi mambo tuliyoainisha na kuongeza mambo mengine kwenye shughuli utakazo chagua kufanya kulingana na mazingira yako. Tunatarajia utafurahia kushirikisha jamii katika harakati za kudai elimu kwa wasichana. Tafadhali tujulishe jinsi utakavyo tekeleza shughuli hizi tunatarajia kusikia zaidi kutoka kwako!

Tunashauri kabla ya kuchagua shughuli, kila mtu katika timu ya mipango asome maelezo ya Kampeni na karatasi ya kazi za kampeni inayopatikana kwenye kiti ya kuchukua hatua na Utetezi ili ujifunze masuala yatakayoshughulikiwa wakati wa kampeni.

## SHUGHULI ZA KAMPENI ZINAZOPENDEKEZWA.

### Shughuli za kijamii.

**Majadiliano ya bango:** shirikisha watu na vikundi vidogo katika majadiliano kwa kutumia bango na mwongozo wa majadiliano kwa njia ya mabango linalopatikana kwenye Kiti hii. Wewe, watumishi wengine na wanaharakati wa jamii au wakujitolea mnaweza kushiriki, watu katika eneo ambalo kuna ushawishi wa haraka kama vile (wanafamilia, marafiki, na majirani), pia husisha watu wengine katika jamii yako. Unaweza kuhamasisha mazungumzo ya haraka na watu binafsi; au wezesha majadiliano ya vikundi. Katika matukio hayo yote, ni muhimu kufanya mazoezi kabla ya utekelezaji. Lengo la mjadala huu ni kuibua mawazo mapya kuhusu tunavyoweza kuwasaidia wasichana kubaki shuleni. Maswali ni njia nzuri ya kuwafanya washiriki waweze kufikiri, tafadhali tumia njia hii na ujitahidi kufanya majadiliano zaidi badala ya kuwasilisha mada au kutoa hotuba – Kwa kufanya hivyo itafurahisha, itavutia na kushirikisha!

**Michezo ya kuigiza katika kijamii:** ,wezesha vikundi vya maigizo katika jamii kufanya majadiliano juu ya elimu ya wasichana. Michezo ya kuigiza katika jamii ni njia inayo tumika katika kuvunja ukimya na kushirikisha jamii katika kujadili mada nyeti. Hadithi inayowasilishwa kwa njia ya maigizo inasaidia kuleta mguso kwa jamii na kuongeza ufahamu wa kina katika masuala husika. Aina yoyote ya sanaa, ina nguvu ya kuhamasisha jamii kuchukua hatua.Tafadhali angalia dondoo zifuatazo ili kuongeza ufanisi katika michezo ya kuigiza: 1) kuwepo na mwingiliano ulio huru kati ya watazamaji na wezesha majadiliano katikati ya matukio, kwa kutumia maswali yanayo wachochea watazamaji kufikiri; 2) Andaa muziki na ngoma kabla na baada ya maigizo, kwani watu wanashiriki na kujifunza vizuri wakiwa na furaha; 3) Endesha tukio hili kwa takribani dakika 30 ili watu waendelee kujihusisha na kushiriki kikamilifu.

Unaweza kusaidia vikundi vya maigiza kwa kupitia makala ya maudhui ya mchezo wa maigizo na maswali ya majadiliano, tafuta mwezeshaji mzuri, Angalia wakati wanafanya mazoezi na toa mrejesho, tafuta maeneo katika jamii yakufanyia michezo ya kuigiza ambayo watu wengi wanaweza kufika.

**Majadiliano ya Jamii:** wahamasishe wanajamii wakusanyike pamoja ili kujadili njia zitakazo hakikisha wasichana kubaki shuleni. Unaweza kuamua juu ya idadi ya watazamaji kulingana na eneo ambalo mazungumzo yatafanyika (k.m., chini ya mti, ofisi ya kiongozi wa mtaa, kwenye kijiwe cha kahawa, ukumbi wa kanisa, nk). Inashauriwa kuwakaribisha watu wa aina mbalimbali wanawake, wasichana, wavulana, viongozi wa jamii, walimu, viongozi wa dini, Mashirika ya kijamii, watoa huduma n.k .Kwa kufanya hivyo utakuwa na sauti tofauti zinazowakilishwa na kufanya majadiliano kuwa bora. Tafadhali tayarisha mazungumzo yako mapema kwa: kupanga muda na mahali, kutuma mialiko, panga ajenda, mwongozo wa majadiliano, Tafuta na muandae atakaewezesha majadiliano mapema .

Fungua majadiliano kwa kuwasalimia washiriki, tambulisha mada na madhumuni. Anzisha mazungumzo kwa kuuliza maswali yanayoibua mawazo. Mwezeshaji anapaswa kuhakikisha michango inatoka kwa washiriki tofauti, hasa wasichana, kutoka katika chumba cha majadiliano. Ikiwa unaweza kuandaa chombo cha habari itakusaidia kufikia hadhira kubwa.

Mwishoni mwa majadiliano, hitimisha dondoo muhimu zitokanazo na mjadala, ainisha ahadi na chagua mtu wa kuongoza mchakato wa ufuatiliaji.

**Michezo na mashindano:** Andaa michezo na mashindano kwa watoto na / au watu wazima. Unaweza kufikiria michezo ya bao, mpira wa pete, mpira wa miguu, mashindano ya baiskeli, mieleka nk tumia fursa hii ili kuhakikisha kila mtu ana ana mtizamo chanya wakati wa kujadili masuala yatakayo hakikisha wasichana wanakamilisha elimu ya juu. Ili kuchanganya, unaweza kuwa na michezo kwa wasichana ambayo kwa asili hufikiriwa kuwa ni ya wavulana na kinyume chake. Wazo ni kuvunja ubaguzi wa kijinsia na pia kuhamasisha wasichana na jamii kuamini kuwa wasichana wanaweza kuwa na ndoto kubwa na kufanya chochote!

**Maandamano ya jamii:** Ni njia yenye nguvu na inayoweza kuleta mwitikio mkubwa kuhusu suala husika. Unaweza kufikiria kuandaa maandamano mnamo Novemba 25 ili kuonyesha mwanzo wa kampeni na kauli mbiu ya mwaka huu, au siku yoyote ambayo ni muafaka kwako. Wakaribishe na uhakikishe ushiriki wa wafanyakazi wako, mashirika rafiki, viongozi wa jamii, wanafunzi, walimu na washiriki wengine wanaopenda. Gawa utepe wa zambarau kwa washiriki ili wavae wakati wa maandamano. Wakati wa maandamano waandamanaji wanaweza kuimba au kupiga kelele kuhusiana na kauli mbiu ya kampeni (Kila msichana ana thamani! Je! Utachukua hatua gani ili Kuwawezesha Wasichana kubaki Shuleni?). Ikiwezekana karibisha bendi au ngoma za asili ili kuongoza maandamano hizi ni njia zinazoweza kuleta mvuto kwa wanajamii.

## Kushirikisha Vyombo vya Habari katika kampeni

Vyombo vya habari ni njia nzuri ya kuwasilisha ujumbe muhimu kwa watu wengi katika maeneo makubwa kijiografia. vinaweza kuwa na ushawishi mkubwa kwa watu jinsi wanavyofikiria na kutenda. Unaweza kutumia redio, TV, magazeti, simu ya mkononi au mtandao ili kuimarisha kampeni ya siku 16. Zifuatazo ni baadhi ya shughuli za vyombo vya habari zinazoweza kutekelezwa:

- **Mkutano na Waandishi wa habari:** Karibisha vyombo vya habari vilivyopo katika jamii yako, washirikishe ujumbe muhimu juu ya elimu ya msichana na wito wa kuhakikisha ongezeko la wasichana kubaki shuleni. Gawa waraka kwa waandishi wa habari unaoelezea suala hili, kwa nini ni muhimu, kinachotokea ndani ya eneo lako na mapendekezo ya hatua za awali zinazo weza kuchukuliwa. Weka nukuu za wasichana, walimu au mwanaharakati wengine. Mwishoni mwa mkutano wa waandishi wa habari, uwe tayari kujibu maswali kutoka kwa waandishi wa habari.Hakikisha kwamba tangazo lako linafaa ili uweze kupata mwitikio mkubwa kutoka kwenye vyombo vya habari mbalimbali kwaajili ya suala hili. Unaweza pia kutumia njia hii ili kupanua kampeni yako na shughuli zilizopangwa. Kumbuka:

kampeni ni fursa muhimu ya kushirikiana na mashirika mengine yanayofanya kazi zinazofanana na shirika lako. Mkutano wa waandishi wa habari kwa kushirikiana na mashirika rafiki utaweza kuongeza mwitikio mkubwa katika kuwakilisha ujumbe.

- **Maonyesho ya Televisheni na majadiliano ya redio:** shirikisha vituo vya redio au TV ili kuandaa vipindi vya majadiliano juu ya elimu kwa wasichana. Mwongoza kipindi anaweza kuboresha majadiliano kwa kualika jopo la wataalamu (wanaharakati wa haki za wanawake, wataalam wa elimu na wasichana walioathirika na suala hili nk). Inaweza kutangazwa mubashara ili watazamaji waweza kupiga simu ili kushiriki katika mazungumzo.

- **Makala katika magazeti:** kwa kutumia maudhui yaliyomo kwenye kauli mbiu ya Kampeni kama mwongozo unaoweza kuwasaidia wanaharakati kuandika makala pia kuchapishwa katika magazeti ya ndani ya nchi. Makala zinaweza kuwa katika mfumo wa maoni yaMhariri, barua kwa mhariri au makala ya wanajamii. Unaweza pia kuandaa makala maalum ya kampeni na kuonyesha wasichana ambao wako shuleni na wanafanya vizuri. Hakikisha makala zote zinatoa ujumbe unaoleweka kuhusu kuhakikisha wasichana wanabaki shuleni.

- **Kampeni za Ujumbe Mfupi wa Maneno (SMS):** Matumizi ya simu za mkononi yamepanuka; kuna ongezeko la idadi ya watu wanaotumia simu za mkononi na wameunganishwa kwenye mtandao. Kampeni ya SMS ni mojawapo ya njia yenye ufanisi ambayo inaweza kutumika kutangaza masuala yetu kwa watu wengi katika eneo kubwa. Ujumbe Mfupi wa Maneno una kiwango maalum cha maneno unayopaswa kuandika, andika ujumbe unaoeleweka na mfupi. Kumbuka kutumia lugha rahisi na epuka vifupisho vya maneno.

- **Kampeni kwa Kutumia Mitandao ya Jamii:** Majukwaa ya mitandao ya jamii yanazidi kuwa maarufu kwa kuhamasisha jamii na kupashana habari juu ya masuala mbalimbali. Tumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kuongeza ufahamu juu ya elimu ya wasichana, hakikisha unatumia kurasa nyingine za mitandao ya jamii ambayo zina watumiaji wengi.

Mtandao wa Kuzuia ukatili wa Kijinsia katika siku 16 utashirikisha mitandao ya kijamii itakayofanyika tarehe 25 Novemba, Desemba 1 na Desemba 10. Angalia hadithi za wanachama kwenye mtandao wa tweeta juu ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ambazo zitarushwa wakati wa kampeni. Tafadhali tutumie taarifa mpya za shughuli zako kwenye info@preventgvhafrica.org ili tuweze kushirikishana kwenye kanda yote..

Wasiliana nasi kupitia @GBVNet na Facebook (Mtandao wa Kuzuia ukatili wa kijinsia)

**Furaha Kampeni!**